

**Becoming secure, strong
and independent**
Family resources

Kuwa mwenye salama, hodari na huru

Rasilimali za familia

Mfumo wa Kujifunza Miaka ya Mapema (Early Years Learning Framework) ni mfumo wa kitaifa wa kujifunza unaotumika katika shule za mapema na huduma zote za utotoni. Inaongoza ufundishaji na kujifunza na matokeo matano ya kujifunza ambayo husaidia watoto kuwa wanafunzi hodari na wenye uwezo.

Matokeo ya Kujifunza 1 ni juu ya watoto kuwa na hisia yenyewe nguvu ya nafsi. Hii husaidia watoto kujiamini wao ni nani na tamaduni zao. Ikiwa watoto wanajisikia salama na wanajua kuwa ni wa familia, jamii na utamaduni, wanaweza kuwa na ujasiri katika njia wanavyojifunza.

Kwa habari zaidi juu ya Early Years Learning Framework nenda kwa:
<https://www.dese.gov.au/collections/translations-belonging-being-and-becoming-early-years-learning-framework-australia>

Huduma ya Mkalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji habari zaidi tafadhalni wasiliana na shule ya mapema au huduma ya utotoni ya mtoto wako. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia katika swali yako tafadhalni pigia simu kwa Huduma ya Mkalimani wa Simu kwa 131 450 na uombe mkalimani katika lugha yako. Opereta atapiga nambari ya simu unayotoa na kupata mkalimani kwenye laini kukusaidia na maswali yako. Hautatozwa kwa huduma hii.

Kujifunza shulenii

Kujifunza kwa mapema

Hisia yenye nguvu ya nafsi inamaanisha:

Watoto wanajua jinsi ya kushiriki, kujifunza kutoka, kuheshimu na kuwepo na wengine

Watoto wanajua ni wa familia zao, jamii na utamaduni wao

Watoto wanajua watakuwa sawa na wanaweza kudhibiti mabadiliko na hisia

Watoto wanajua ushawishi wao juu ya watu, mahali na ujifunzaji wao

Wanafunzi huwasiliana na kushirikiana na vikundi anuwi vyatkitamaduni (Sehemu zote za masomo)

Wanafunzi wanajua juu ya tabia ya maadili na kukuza uwezo wa kibinafsi na kijamii (Sehemu zote za masomo)

Wanafunzi wanajiamini katika kusaidia afya yao ya kimwili na ustawi (Somo: Masomo ya kimwili)

Wanafunzi wanaweza kujua, kuheshimu na kusherehekea tamaduni zingine (Sehemu zote za masomo)